

NANI MWANAMKE?

Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake

(Kitabu cha Kwanza)

Na

Shamte Kilalile

YALIYOMO

HAKIMILIKI	3
KIDOKEZO.....	1
UTANGULIZI	2
SURA YA KWANZA.....	5
SEHEMU YA KWANZA.....	10
SURA YA PILI.....	11
SURA YA TATU.....	15
SURA YA NNE	21
SURA YA TANO	26
SEHEMU YA PILI	32
SURA YA SITA	33
SURA YA SABA.....	37
SURA YA NANE	41
SURA YA TISA	44
MUHTASARI	47
KIDOKEZO CHA KITABU KIJACHO	48
KUHUSU MWANDISHI.....	50
KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE.....	51

HAKIMILIKI

Hakimiliki© 2022 Shamte Juma Kilalile

Haki zote zimehifadhiwa. Kwa malipo ya gharama husika umeruhusiwa kusoma kitabu hiki. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupakua au kusambaza bila idhini ya kimaandishi kutoka kwa Mwandishi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakayekiuka.

Yaliyomo kwenye kitabu hiki yametokana na fikra na mawazo ya Mwandishi na wala yasitumike kama sehemu ya ushauri wa kisheria au binafsi. Ni jukumu lako kuchunga mwenendo na tabia zako binafsi.

Shamte J. Kilalile

Kijichi, Dar Es Salaam

Tanzania

KIDOKEZO

Ukimuuliza mwanamke yoyote kuhusu sifa za mwanaume anayevutiwa nae au anayependa kuwa nae, hutakosa majibu haya;

1. Mwenye hofu ya Mungu/Mcha Mungu
2. Mwenye pesa/tajiri
3. Mwenye upendo/mapenzi
4. Mwenye kujali
5. Mwenye mvuto/muonekano mzuri
6. Mwenye heshima/sio msaliti

Hizi ni baadhi ya sifa za mwanaume bora (*good man*) na mwenye mamlaka (*dominant*). Lakini uhalisia wa mambo ni kuwa kwenye mahusiano kuna;

1. **Wanaume watawaliwa (*submissive*):** Kuna wanawake wanapenda kuwa kwenye mahusiano na wanaume wanaoweza kuwatawala.
2. **Wanaume wenye tabia mbaya:** Kuna wanawake wanavutiwa na wanaume ambao licha ya kuwatesa lakini hawaachani nao.
3. **Wanaume wasaliti:** Kuna wanawake wanapenda wanaume ambao licha ya kujua wanawasaliti lakini hawaachani nao.
4. **Wanaume wenye mvuto wa kawaida/hawana mvuto kabisa:** Kuna wanawake ambao wanapenda wanaume wenye muonekano wa kawaida kabisa au wale ambao jamii inawaona wana sura mbaya.

Kwanini?

Jawabu la swali hili liko kwenye kitabu hiki.

UTANGULIZI

Nani mwanamke?

Hakuna jibu la moja kwa moja juu ya swali hili kwasababu majibu yake inategemea ni nani anayeulizwa na katika mazingira gani swali hili limeulizwa. Baadhi ya majibu ni;

1. wapo wanaume wanaosema mwanamke ni chombo cha starehe,
2. wapo waandishi waliondika vitabu na kusema ni kiumbe kisichoeleweka na
3. wapo wanaharakati wasemao ni kiumbe chenye nguvu na jasiri mwenye uwezo wa kufanya sawa na anayoyafanya mwanaume.

Licha ya utofauti huu wa majibu, wote tunakubaliana ya kuwa kimaumbile na namna walivyoumbwa, **wanawake ni viumbe vya kihisia (*emotion creatures*) zaidi kuliko wanaume.** Ikiwa wote tunakubaliana katika hili, hii inajulisha ya kuwa;

1. wale wanaume wanaosema wanawake ni chombo cha starehe wakiwa wanajihalalishia kukidhi hisia na haja zao tu, kauli hii itakuwa ya kimakosa kwa sababu wanawake nao wana haki hiyo kama wao na zaidi kwa sababu ya maumbile yao.
2. wale wanaosema ni kiumbe kisicholeweka, kwa upande mmoja kauli yao itakuwa ya sawa kwasababu hisia ni kitu chenye kubadilikabadilika na wanawake hisia zao zinabadilikabadilika kutegemea na hali na mabadiliko kati miili yao. Mfano mwanamke huwa katika hisia tofauti akiwa kipindi cha ujauzito na siku zao za mwezi.

Lakini upande mwingine, wameshindwa kuelewa na kuisoma saikolojia ya mwanamke inavyofanya kazi katika hisia zake. Mfano kuna wakati mwanamke anaweza akasema hapana lakini akimaanisha ndio na kuna wakati akisema hapana anamaanisha hapana. Kuzijua nyakati hizi ndipo kunawapa shida wanaume wengi ndio maana kunaleta kauli mfano wa hii ya kusema ni viumbe visivyoeleweka.

3. ama kuhusu kauli ya wanaharakati, mimi ninaamini kama ambavyo kuna mambo ambayo mwanaume hawezi kuyafanya sawa na mwanamke kadhalika kuna mambo mwanamke hawezi kuyafanya sawa na mwanaume. Na utofauti huu unatokana na maumbile yao ambayo Mungu amewauumba na kumfanya kila mmoja kumtegemea mwenzake.

Na kila ambaye atajaribu kwenda kinyume na kanuni hii atajiletea madhara kwake mwenyewe au kwa familia yake hata kama atajitutumua na kujidai mbele ya kamera, magazeti na vyombo vingine vya habari kuwa anajivunia kuwa hivyo. Nitaishia hapa katika kuwajibu wanaharakati kwa sababu sio lengo la kitabu hiki kufanya hilo.

Inaweza kuwa ngumu kumuelewa mwanamke kwa ujumla wake lakini ni rahisi kumvunjavunja katika vijishehemu mbalimbali na kumuelewa kutegemea na vijishehemu hivyo kwa kuwa msingi wa kauli tuliyokubaliana ya **mwanamke ni kiumbe chenye hisia**, inatupa mahali pa kuanzia.

Katika kuifata na kusimama katika kauli hii ndio nimeandika kitabu hiki cha **Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake** kuelezea vipi hisia za mwanamke zinamuongoza katika kijishehemu au kipengele cha uchaguzi wa mwanaume. Yaani vipi hisia zake zinamfanya kuvutiwa zaidi na wanaume aina fulani kuliko wanaume wa aina nyingine.

Kuvutiwa kuko kwa aina mbili;

1. Kuvutiwa na sifa mbaya
2. Kuvutiwa na sifa nzuri

Ni ukweli usiopingika ya kuwa wanaume na wanawake tunatofautina sana namna tunavyochakata (*processing*) hisia zetu. Baadhi ya aina za wanaume nitakazozitaja kwenye kitabu hiki zitaonyesha kuwa na sifa au tabia mbaya lakini bado kuna wanawake wanavutiwa na kupenda kuwa nao kimahusiano.

Pia kuvutiwa kuko kwa aina nyingine mbili;

1. Kuvutiwa na mtu alivyo
2. Kuvutiwa na kitu alichonacho mtu

Pia baadhi ya aina ya wanaume nitakazozitaja humu huwavutia wanawake kwa namna walivyo lakini pia wapo ambao wanawavutia wanawake kwa vile walivyonavyo.

Kitabu hiki kitakuwa ni kitabu cha kwanza katika mfululizo wa vitabu vya **Nani Mwanamke?** Ninataraji kuandika vitabu vingine kumgusia mwanamke katika vipengele tofauti tofauti kulingana na tabia yao ya kimaumbile.

Walengwa haswa wa kitabu hiki ni wanaume na ninatumai kitawanufaisha zaidi wao japokuwa wanawake nao wanaweza kutoka na faida humu. Kitabu hiki kitawanufaisha wanaume wa makundi mawili;

1. Kwa wanaotarajia kuoa:

- kuepuka kosa kongwe linalofanywa na wanaume la kutanguliza pesa mbele kama kishawishi cha kuwanasa wanawake.
- kujua sifa mbadala za kujipamba nazo mwanaume ili kumpata mwenza wa Maisha yake.

2. Kwa walio kwenye ndoa: kubadilisha tabia au sifa mbaya walizokuwa nazo ili kunusuru ndoa zao.

Lakini pia kitawanufaisha na wanawake kwa namna kuu tatu;

1. **Kujua sababu za kwanini wanavutiwa na aina hizi:** Tafiti zinaonyesha ya kuwa hata wanawake wenyewe, wengi wao hawajui ni kwanini wanavutiwa zaidi na aina hizi.
2. **Kujiepusha na aina ya wanaume ambao wana sifa au tabia mbaya.**
3. **Kuwapa wapenzi wao kitabu hiki:** Mwanamke anaweza kukitumia kitabu hiki kama njia ya kutuma meseji kwa mpenzi wake ambaye kuna sifa amezipoteza zilizomfanya awali kuvutiwa nae.

Karibu uungane nami.

SURA YA KWANZA

UTU

(*Personality*)

Kwa mujibu wa kamusi ya Tuki ya Kiswahili-Kiingereza linatafsiri neno la kiingereza *personality* kuwa ni haiba. Kwa kuwa neno hili la kiingereza limetokana na neno lingine la kiingereza *person* likiwa na maana ya Mtu, nimeona niipe sura hii kichwa cha habari **Utu** likimaanisha *personality* kukidhi haja niliyokusudia kuielezea katika sura hii kuliko kutumia neno haiba ambacho ni kijisehemu cha Utu.

Maana ya utu inakusanya vitu vitatu vinavyomjenga mtu;

1. Hali ya kiuchumi: kazi, pesa, gari, nyumba n.k.
2. Tabia: ucheshi, gubu, kujali, nongwa, kujionyesha, kujisifu, umakini, n.k.
3. Hisia: upendo, huruma, hasira, n.k.

Mwanamke huvutiwa na mwanaume kutokana na aidha hali yake kiuchumi au tabia zake au hisia zake. Inaweza kuwa kimoja wapo kati ya hivi au viwili au vyote vitatu.

Kama ukimuuliza mwanamke swali hili, je angetenda kuwa na mwanaume mwenye muonekano mzuri (*handsome au six packs*) au mwanaume mwenye pesa? Bila shaka jibu utakalolipata ni mwanaume mwenye pesa. Na kama utampata atakayechagua muonekano bila shaka atatengeneza swali lake ili apate mwanaume mwenye muonekano na pesa. Nilijaribu kumuuliza swali hili mwanamke mmoja, alipotaka kupata mwanaume mwenye sifa zote mbili alitengeneza swali lake na kuniuliza, “kwa hiyo Shamte huyu mwanaume *handsome* hana pesa hata kidogo?” Nilicheka kisha nikamjibu kuwa hana na msingi wa swali ni kuwa kila mwanaume ana sifa moja tu ambayo anatakiwa kumchagua. Hatimaye alichagua mwenye pesa bila kupepesa.

Kwanini mwanamke anaweza kutengeneza swali lake ili apate vyote viwili? Ni kwasababu muonekano una nafasi yake kwenye mapenzi hasa pale linapokuja suala ya kujionesha (*showing off*) kwa shoga zake pindi anapotoka na mume wake matembezini. Ila pale chaguo linapotakiwa kuwa moja, mwanamke hutanguliza pesa kuliko muonekano wa mwanaume.

Kwanini wanatanguliza pesa? Ni kwa sababu wanawake wanavutiwa zaidi na utu (*personality*) wa mwanaume kuliko muonekano wake.

Pesa ni sehemu ya utu ndiyo maana kuna msemo wa Kiswahili usemao **mtu ni pesa**. Ama kuhusu sura, sura siyo sehemu ya utu ndio maana wanawake wana msemo wao usemao **sura hata mbuzi anayo**. Unaweza kuonekana ni msemo fulani wa kebehi au kimbea au uko kiutani ila ukijua ufanyaji kazi wa saikolojia ya wanawake na hisia zao utagundua ya kuwa wanamaanisha wanachokisema.

Ndiyo maaana si ajabu kuona mwanamke akiwa na mahusiano na mwanaume mwenye sura ya kawaida au mbaya¹ lakini anazo pesa na akudumu naye. Ila ni nadra kuona wanawake wako kwenye mahusiano na wanaume wenye sura nzuri lakini hawana pesa na wakadumu bila ya wanawake hao kutafuta ‘wafadhili’ (*sponsor*) nje. Sababu zinaweza zikawa;

- Mwanaume mmoja anakuwa ni wa mtoko na mwengine ni wa kuchuna au,
- Mwanaume mmoja yuko na mapenzi naye ya dhati na mwengine yuko nae kwa lengo maalumu.

Jua ewe mwanaume, muonekano wako haulipi gharama zake za kimaisha (*Your look doesn't pay her bills*) na wala si kigezo kikubwa sana cha kumvutia mwanamke ila utu ni kigezo kama ambavyo tutakuja ona kwenye kila aina ya mwanaume hapo mbeleni.

Kuna msemo wa kiingereza usemao *first impression matters* wakiwa na maana ya kuwa kuna umuhimu mkubwa sana namna unavyojiwasilisha kwa watu kwa mara ya kwanza. Kanuni hii ni muhimu si tu kwenye biashara na kazi bali pia kwa wanawake.

Kosa kubwa wanalolifanya wanaume wengi ili kuwanasa wanawake ni kujionyesha kuwa ni watu wenye pesa; wanawatoa kwenda sehemu za gharama, watawanunulia vitu vya ghali, na mfano wa hayo. Wasichotambua ni kuwa kitendo hiki kinapofanywa kwa mara ya kwanza kinachakatwa (*processing*) na kupewa tafsiri tofauti kwenye vichwa na fikra za wanawake. Wakati wanaume wanafikiri mnaso, wanawake wanafikiri wamepata buzi la kuchuna.

Njia ya kutanguliza pesa mbele ili kumnasa mwanamke inafanya kazi;

1. Kama mwanaume unatafuta mwanamke wa ‘huduma ya haraka’- machangudoa/wadangaji
2. Kama mwanaume unatafuta mwanamke wa kupitisha siku (*one-night standing*).
3. Kama mwanaume unatafuta mwanamke wa kustarehe nae tu na kuhonga kwako sio ishu.

Ila kama unatafuta mwenza wa Maisha, tumia njia sahihi kwa kufata hatua hizi;

1. Jijue wewe ni nani
2. Jua unataka mwanamke wa aina gani
3. Jua mwanamke wa aina unayotaka anapatikana wapi
4. Ongea lugha yake

¹ Nasema sura mbaya katika mazingira ya kueleweka na utumikaji wa neno wala sio katika ukosoaji wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Ubaya au uzuri wa sura ya mtu uko kwa yule anayemuangalia. Mtu anaweza kuwa mbaya kwa mtu fulani lakini ni mzuri kwa mwengine.

Tufafanue hatua hizi kwa mfano:

1. Jijue wewe ni nani: Mfano wewe ni mfanyabiashara na unapenda mambo yanayohusu biashara
2. Jua unataka mwanamke wa aina gani: Unataka mwanamke ambaye anajihusisha na biashara kama wewe
3. Jua mwanamke wa aina unayotaka anapatikana wapi: Kongamano, semina na warsha zinazohusiana na biashara
4. Ongea lugha yake: Usikimbilie kutongoza na kuhonga moja kwa moja kama wafanyavyo wanaume wengi wanapona wanawake barabarani. Mfano umekutana na mwanamke aliyekuvutia kwenye kongamano la biashara, unaweza kuanzisha mada juu ya kilichoongelewa na mtoa mada fulani aliyepita jukwaani. Wakati mwanamke anapochangia mada kutakuwezesha kujua upeo wake, kujua hisia zake pale unapompa changamoto ya maswali kwenye mada tata. Au unawezesha kuonyesha kutaka kujua alivyoingia kwenye biashara, changamoto anazozikabili na toa ushauri kwenye changamoto zake (kuwa *smart* hapa kwasababu kwenye kichwa cha mwanamke unapitia mchakato wa kutafsiriwa wewe ni mwanaume wa aina gani). Wanawake wanapenda wanaume *smart* kuliko wao na wenye kujali wanachofanya.

Fata hatua hizi na utakuwa kwenye nafasi ya kutafsiriwa kwenye fikra na hisia za mwanamke kama mwanaume makini. Utanishukuru baadae.

Tatizo ni kuwa hatua hizi huzingatiwa na kufatwa kwa umakini na wanaume wenye tabia ya ukware (umalaya). Mwanaume mweye tabia hii ikiwa atajua mwanamke anayemtaka ni mtu wa dini na anahudhuria nyumba fulani ya ibada, naye ataanza kujifanya ni mtu wa dini na kwenda kwenye nyumba hiyo.

Na huwa hawaanzi kumtongoza bali wanaanza kujihusisha katika yale ambayo mwanamke huyo anajihusisha na kuyapenda; ikiwa ni mwanamke anajihusisha na kwaya naye atajihusisha kwenye kwaya au kupiga kinanda na ikiwa ni kujitolea kwenye shughuli za kijamii kama kusaidia mayatima, naye atajihusisha humo. Lengo lake ili;

1. Kutengeneza uaminifu kwa mwanamke,
2. Kutekengeneza picha ya mpenzi na mume bora,
3. Kuonyesha kujali kile ambacho mwanamke anafanya.

Shida inakuja pale mwanamke anapomuamini na akampa anachokita, mwanaume anaingia mitini na kutoa sababu nyingi kama ametingwa na shughuli.

Sikushauri kuchezea hisia za wanawake kiasi hiki.

Vile wanaume wanavyojiwasilisha kwa mara ya kwanza (*first impression*), wanawake huvutiwa na hatimaye kuwagawa wanaume katika makundi mawili;

1. Mwanaume mwenye sifa ya Mpenzi
2. Mwanaume mwenye sifa ya Buzi (mfadhili)

Wanaume wenye sifa ya Mpenzi wako makundi manne;

1. Mtongozaji (*Seducer*)
2. Chakaramu (*Bad boy*)
3. Msanii (*Artist*)
4. Adivenchara (*Adventurer*)

Wanaume wenye sifa ya Buzi wako makundi manne pia;

1. Dadi (*Daddy*)
2. Sponsa (*Sponsor*)
3. Bwege/Zoba (*Regular man*)
4. Toi (*Toy boy*)

Kutokana na kukosa maneno ya Kiswahili ambayo yanaweza kutafsiri maneno ya kiingereza yaliyopo kwenye mabano ili kuelezea aina hizo za wanaume na kuleta mvuto, nimeonea niyatohoe kama yalivyo na kutamkwa kutoka kwenye lugha ya kiingereza. Kama ningetumia jina la ‘**Mtu mwenye vituko**’ kutafsiri jina **Adventurer** lingelea tafsiri tofauti kwa msomaji au asielewe mpaka atapofika kwenye sura maalumu inayomhusu mwanaume wa aina hii. Mfano wa majina mengine ni *Daddy* (nimeona ugumu kutafsiri kama **Baba**), *Toy Boy* (kama **Mdoli au Mwanasesere**) na *Regular man* (kama **Mwanaume wa Kawaida**) kwa sababu ya kukosa mvuto.

Kadhalika jina **Sponsa** nimelitoa kwenye neno la kingereza lenye kutamkwa sawa na hivyo linavyotamkwa kutoka kwenye kiingereza (**Sponsor**) kuwakilisha aina fulani ya wanaume utakaokuja kuwaona huko mbele kwenye sura yake maalumu. Lengo la kutumia jina Sponsa kama Kiswahili nimeona itakuwa rahisi kwa msomaji kuelewa kutokana na umarufu wa jina hili kwa namna linavyotumika kwenye muktadha (mazingira) fulani kuwakilisha wanaume fulani.

Tafsiri ya majina *Seducer* kama **Mtongozaji** na *Artist* kama **Msanii** nimeona tafsiri hizi zitafaa kufikisha lengo langu kueleza wanaume aina hizo.

Kutofautisha kati ya mwanaume MPENZI na mwanaume BUZI ni namna ambavyo wanawake wanavyowaitikia (*respond to them*) haswa kwenye suala la kujamiana;

- 1 . Mwanamke anatoa tendo la ndoa kwa mwanaume MPENZI haraka sana.
- 2 . Mwanamke anakuwa mgumu kwenye hilo kwa mwanaume BUZI kwa sababu kuu mbili;
 - kumchuna au
 - kumpima kama ‘Buzi’ anamuhadaa au lah. Wanawake washajua silaha ya wanaume kuwahadaa ni pesa, hivyo mwanamke anapona mwanaume anatanguliza pesa mbele anatafsiri huo ni mtego kwa hiyo anabana kutoa tendo.

Sura nne zinazofata nitaanza kuongelea wanaume kwenye kundi la MPENZI mmoja baada ya mwengine.

SEHEMU YA KWANZA

Mpenzi

1. Mtongozaji (*Seducer*)
2. Chakaramu (*Bad boy*)
3. Msanii (*Artist*)
4. Adivenchara (*Adventurer*)

SURA YA PILI
MTONGOZAJI
(Seducer)



Linapokuja suala la kujua tabia za wanawake na yale wanayoyapenda, wanaume wamegawanyika makundi mawili;

1. **Wawajuayo wanawake kinagaubaga:** Hawa wanawakilishwa na kauli mojawapo wazisemazo wanawake, “mwanaume ananijua kama amenizaa”
2. **Wasiowajua wanawake kabisaaaa:** Hawa wanawakilishwa na kauli nyingine ya wanawake, “mimi hata si muelewi yule mwanaume”. Anachomaanisha mwanamke hapa sio kwamba hamuelewi kweli {ukweli ni kuwa ashaelewa mwanaume aliyekuwa naye ni ‘kichwamaji’ (*dumb*)} bali anachomaanisha ni kwanini mwanaume wake hamuelewi.

Wanaume aina ya Watongozaji wako kundi la kwanza.

Kiasili kila mwanaume ni mtongozaji lakini kwa dhumuni la kitabu hiki nimekopa neno hili maalumu kuwakilisha aina hii tu.

Mtongozaji ni aina ya mwanaume ambaye anamfanya mwanamke ahisi uwanamke wake (*feeling sexy/womanhood*). Mwanaume wa aina hii ni kana kwamba alishawahi kuzaliwa mwanamke katika Maisha yake ya zamani kabla ya kuwa mwanaume.

Mtongozaji yuko makini kujua nini mwanamke anapenda na lengo lake hasa ni kumfurahisha ili apate anachotaka, ambalo ni kujamiana nae. Nathubutu kusema ya kuwa mwanaume mkware (mwanaume mwenye tabia ya umalaya) na Mtongozaji ni sawa.

Moja ya kitu wanachopenda wanawake ni maneno mazuri/matamu. Mtongozaji analijua hili hivyo anajua nini cha kusema, wakati gani wakusema na namna ya kusema. Mtongozaji anajua na kuitendea vyema kanuni ambayo ninaita **Sema, Sema tena, Sema vizuri** (*Say it, Say it again, Say it better*). Wahanga katika hili ni wanawake ambao wamelala na wanaume ambao ni mara yao ya kwanza kuonana nao au kutoka nao *out* kisha ukawasikia wakijitetea mfano wa kauli hii “hata sijui mwaya, sijui yule kaka aliniekea madawa ya kulevya, sijui aliniloga, maana najikuta niko chumbani kashanivua nguo”.

Kitu kingine wanachopenda wanawake ni ndoa. Na lengo lingine la Watongozaji ni watoto na sio kuoa. Kwa hiyo, Watongozaji wanajua nini cha kutenda na wakati gani wa kutenda ili kutimiza lengo lao. Wanawake wanapenda ndoa kwa sababu kuu mbili;

1. Heshima anayopata kwa jamii kwa kuwa mke wa mtu. Hili ni maarufu sina haja ya kulielezea sana.
2. Kutoka nyumbani kwao. Hili nilifafanue kidogo. Mwanamke, kwa sababu zozote atakazo kuwa nazo kichwani mwake iwe;
 - kutaka kutoka kwenye familia anayoishi nayo kwa sababu inamtesa au
 - kutaka kuwa na uhuru au
 - hataki tu kukaa kwao

na ikiwa hana njia ya itakayomuwezesha kuondoka-mfano ajira, ndoa kwake inakuwa njia ya mkato. Ukinzani kati ya hitaji la mwanamke na lengo la Mtongozaji linaanzia hapa. Mtongozaji anajua ndoa inamaanisha nini kwa mwanamke (sababu ya kwanza hapo juu) na ikitokea akajua udhaifu mwingine wa hitaji la mwanamke (sababu ya pili), ni fursa kwake na ndio unaweza kusikia mfano wa kauli hii mwanaume Mtongozaji akiisema; **nizalie nitakuoa**.

Changamoto hapa kwa mwanamke inakuwa ameshakolea kwenye mapenzi na anahitaji sana kuondoka kwao. Hatimaye anaachia ‘goli wazi’ na Mtongozaji anapata anachokitaka. Suala la mtoto atakapopatikana na vurugu za kisheria zitakazokuja kutokea za malezi ya mtoto, hili ni suala lingine na sio dhumuni la kitabu hiki kuliongelea.

Kadhalika watongozaji wako tayari kufanya mambo ambayo mwanaume wa kawaida anaweza kuyaona hayaingii akilini kuyafanya. Bila shaka umeshawahi kusikia visa vya wanawake kuachwa baada tu ya mwanaume kutoa mahari. Tumeona lengo la mtongozaji ni kujamiana na mwanamke anayemtaka na akishafanikiwa anaingia mitini. Kwa hiyo huwa hajali atatumia njia gani ili afanikiwe hata ikibidi kupoteza mahari yake au kujifanya mtu wa ibada kama tulivyoona kwenye tabia ya mwanaume malaya.

Changamoto nyingine ya wanaume watongozaji ni wabobevu wa ‘kupasha viporo’. Anaweza akamuacha mwanamke kisha akamrudia tena kwa maneno matamu ya kuomba msamaha, kubembeleza na mbinu kedekede na hatimaye mwanamke akalala nae tena kisha huyooo anamuacha tena. Wanawake ambao wamekumbwa na mikasa hii huwa wanajiona wapumbavu kufanywa wajinga kwa mara nyingine tena ila ukweli ni kuwa ni ngumu sana kwao kuwakatalia na kukabiliana na vishawishi vya wanaume wenye sifa ya utongozaji.



Hawa jamaa wako vizuri sana.

Nini Cha Kujifunza Kwa Mtongozaji

1. Wanawake wanapenda maneno mazuri kwa hiyo inalipa kuwa na maneno mazuri kwa mwanamke umpendae.
2. Ni sawa kumjua mwanamke tabia na hisia zake ili kumfurahisha, kumridhisha na kujua namna ya kuishi nae.

Nini cha Kuacha kwa Mtongozaji

1. Si busara kucheza na hisia za mwanamke.
2. Si sawa kuwa na tabia ya ukware (umalaya).

SURA YA TATU
CHAKARAMU
(*Bad Boy*)



Kamusi ya Tuki ya Kiswahili-Kiingereza inatafsiri neno Chakaramu kama *naughty person* (mtu mtundu). Kwa dhumuni la kitabu hiki neno Chakaramu nitalilinganisha sawa na neno la kiingereza la *Bad Boy* zaidi kuliko *naughty person*.

Kama ushawahi kusikia wanaume ambao wananyanyasa wanawake kijinsia basi ni aina hii ya wanaume. Mwanaume chakaramu au *Bad Boy* ni aina ya mwanaume ambaye furaha yake huipata katika kumpiga, kumdhuru au kumnyanyasa mwanamke wake. Ajabu ni kuwa huyo mwanamke anayenyanyaswa haachani na mwanaume wa sampuli hii.

Na ukimuuliza kwanini hamuachi, atakujibu anampenda.

Na ukimuuliza kwanini anapigwa na kunyanyaswa kiasi hicho, atamtetea kwa kusema yeye ndiye mwenye makosa au mume wake amekosea tu kwa bahati mbaya na hakukusudia kumuumiza kiasi hicho.

Bila shaka ushawahi kuona wanawake wa aina hii au kusikia kauli zao mfano wa hizi. Na huwenda uliwaza moja kati ya haya;

1. Inawezekana hawa wanawake wamelogwa au,
2. akili zao haziko sawa au,

3. wanaume zao wamewatishia ikiwa watasema ukweli wa wanayofanyiwa

Unaweza kuwa sahihi kwani nami nilikuwa kwenye mawazo hayo hayo mpaka nilipokuja kukua kiakili kidogo nikagundua sababu zingine zinazofanya hawa wanawake kubaki na wanaume sampuli hii na wewe huwenda ushawahi kuzifikiria au kuzisikia. Sababu hizi ni;

1. malezi ya watoto au
2. kuhofia kukosa 'soko' kwa sababu ya umri wao kuwa mkubwa,

Nilipokuja kujua tabia na hisia za wanawake niligundua kuna sababu nyingine ya ziada ambayo huwenda hukuwahi kuiwaza au kama ulishawahi basi uliiona haingii akilini. Nayo ni;

- wapo wanawake ambao huvutiwa na aina hii ya wanaume.

Huwenda ukashangaa lakini ndio ukweli.

Na ni katika sababu hii, sura hii ndipo ilipojikita kuwaelezea wanaume wa aina hii.

Chakaramu au *Bad Boy* ni aina ya mwanaume ambaye kitabia ni mhuni na kimuonekano ni mtu hatari. Ni mkorofi kwa watu akiwa nje na ni mnyanyasaji kwa mkewe akiwa ndani.

Mara nyingi *Bad Boy* hukutwa na hatia na kufungwa jela kwa makosa ya kumpiga na kumtesa mkewe wake licha ya baadae kusikia kauli za utetezi za mwanamke huyo kama “ilikuwa bahati mbaya tu au nampenda mume wangu, muachenii”.



Wanaume kwenye kundi hili wana tabia za kibabe, huvaa kibabe, huongea kibabe, huchora *tattoo*, wanywaji wa pombe kupindukia, wavutaji wa sigara na bangi, watumiaji wa madawa ya kulevya na kila sifa ya uhuni ambao sijautaja. Ni aina ambayo kama mwanamke atakwenda kumtambulisha kwa wazazi wake, bila shaka hawezi kukubaliwa.



Mfano, wengi katika wanamziki wa aina ya *rock* ni wanaume wa aina hii.



Au wahuni wa vikundi maarufu kama *gangsters* pia wanaingia kwenye aina hii.



Kwanini Wanawake Wanavutiwa na Wanaume chakaramu au Bad Boys?

1. Kuna uraibu katika hisia za mwanamke kinachochochea kupenda kuwa na mwanaume ambaye ana uwezo wa kuamua kufanya chochote, lolote, wakati wowote na popote. Bad Boy ni katika aina ya wanaume ambao wanawakilisha mwanaume mwenye mamlaka (*dominant*).
2. Hisia hizi zinaweza kumfikisha mbali zaidi mwanamke mpaka kuwaza mambo yatakuwaje akiwa 'faragha' na mwanaume wa aina hii. Kwanini? Kwa sababu kuna wakati mwanamke anapenda kuwa na mwanaume ambaye ni rafu faragha (*treating rough and dirty*), namaanisha chumbani sio mbele za watu. Na Bad Boy ana uwezo wa kufanya hilo.



Ukiona mwanamke ameachana na mwanaume aina hii kuna moja kati ya haya;

- Mateso yamezidi sana kiasi cha kushindwa kuvumilia au,



- Amesaidiwa na ndugu au watu wake wa karibu kuachanishwa ili kumuokoa na mateso au,



- Yeye ndiye ameachwa

Na lau kama mwanaume huyu akirudi, akaomba msamaha na kuahidi kuacha mateso, (na hata kama mwanaume ataendelea na pombe, bangi na kuwapiga wengine huko nje lakini maadamu anamuahidi hatamtesa huyu mwanamke), kuna uwezekano mkubwa wa kurudiana nae.

Nini Cha Kujifunza Kwa Wanaume Chakaramu au Bad Boys?

1. Wanawake wengi wanavutiwa na wanaume wenye mamlaka (*control/dominant*).
2. Hata kama hawakuambii, wanawake wanapenda wanaume wenye kuwa rafu (*treating rough & dirty*) faragha. Mwanaume kufanya hivyo chumbani wanaitafsiri ni sehemu ya mapenzi. Kufanya hivyo nje na mbele za watu, wanaitafsiri ni udhalilishaji. Kuwa makini usichanganye mazingira.

Nini cha Kuacha Kwa Wanaume chakaramu au Bad Boys?

1. Hakuna ulazima wa kuonyesha mabavu kupitia matumizi ya bangi, pombe, madawa ya kulevya au kuwa na tabia nyingine mbovu.
2. Kuna njia nyingine za kuonyesha mapenzi kwa mwanamke na unyanyasaji si miongoni mwa njia hizo.

SURA YA NNE

MSANII

(Artist)



Ni mara ngapi umeshawahi kusikia mwanamke anamuacha mwanaume kwa sababu ya muigizaji wa filamu?

Ni mara ngapi umeshawahi kusikia mwanamke anamuacha mwanaume aliyekuja nae klabu na kuondoka na mwanamziki?

Sura hii inaangazia ni kwanini wanawake huvutiwa na wasanii.

Sanaa ni neno pana na ndani yake kunaingia mziki, uchoraji, uandishi, uigizaji, upishi, na kazi zingine za sanaa. Hivyo hivyo msanii ni jina pana ambalo ndani yake kunaingia kila mtu ambaye anafanya kazi hizo za Sanaa.

Swali, ni kwanini basi wanawake huvutiwa zaidi na wasanii?

- Je ni umaarufu?
- Je ni pesa?

- Au kuna sababu nyingine zaidi?

Binafsi nimeshawahi kuona wanawake wakiwa kwenye mahusiano na wasanii ambao si maarufu kadhalika hawana pesa za 'kutisha'. Hii ina maanisha umaarufu na pesa vinaweza kuwa ni vishawishi kwa baadhi ya wanawake ila ipo sababu nyingine kinyume na hizo.

Sababu yenyewe ni kuwa wakati wanaume wanavutiwa na wanawake kupitia kiungo cha macho (kuona), wanawake upande wao huvutiwa na wanaume kupitia milango yote ya fahamu/hisia (*sensory organs*); macho (kuona), masikio (kusikia), ulimi (kuonja), ngozi (kugusa) na pua (kunusa). Na Sanaa hugusa hisia za wanawake kupitia milango hiyo. Hebu tudadavue moja baada ya nyingine;


Kuona

Kama ushawahi kwenda kwenye Sanaa za maonyesho ya picha utagundua ya kuwa wauzuliaji wengi ni wanawake. Na kama utawaona wanaume basi ujue wameletwa na wapenzi wao.

Ni mara chache sana wanaume wanakwenda peke yao kwenye maonyesho ya aina hii na sababu ni kuwa wanaume hatuelewi maana ya picha kwa hiyo hatujisumbui kwenda sehemu tusizozielewa. Na ukituona tupo sehemu za aina hii ujue tumekuja kuwaridhisha tu wapenzi wetu ila ukituangualia usoni utaona namna tunavyoboleka.

Mwanaume ananua picha kwa sababu mbili;

1. Kwa sababu mpenzi wake ameipenda
2. Kwa ajili ya ufahali (*prestige*). Mfano picha hii ya Monalisa.



Wanaume hawanunui picha hii kwa sababu wanajua maana iliyokusudiwa na mchoraji (kama wapo wanaojua basi ni wachache sana) ila wanainunua kwa sababu Monalisa ni ghali na ni ishara ya ufahali.

Kinyume chake, wanawake wengi wanaelewa maana ya picha. Wakati mwanaume anaona picha imekologwakologwa ila mwanamke anaona mama amebeba kuni kichwani, mgongoni ana mtoto na baba yuko mbele na chupa ya pombe, halafu utasikia akikuambia, “inasikitisha sana, tafadhali mpenzi usiwe kama huyu baba”. Mwanaume unawaza, *huyu mwanamke anaongea nini!?*

Picha ni Sanaa yenye changamoto sana kuelewa kwa wanaume kama ambavyo ni ngumu wanaume kuwaelewa wanawake. Lakini picha na wanawake vikutana pamoja, vinaelewana. Tatizo hapa inakuwa si picha kama picha bali yule aliyeichora hiyo picha. Si ajabu ukasikia mwanamke akisema, “navutiwa sana na picha za huyu mchoraji, yaani zinagusa kabisa Maisha yangu”.

Kusikia

Katika sura ya pili, niligusia suala la wanawake kupenda kuambiwa maneno mazuri nilipokuwa namzungumzia mwanaume aina ya Mtongozaji. Wanawake wanapenda maneno mazuri si tu kuyasikia kwa wapenzi wao bali wanapenda hata kuyasikia yakiwa kwenye miziki.

Akisikia sauti, tungo na mashairi mazuri ya kimahaba kutoka kwa mwanamziki fulani wa kiume anatamani kama maneno hayo angekuwa anaambiwa yeye moja kwa moja. Kadhalika anawaza itakuaje kuisikia sauti hii kila siku au kutungiwa wimbo wa kimahaba. Njia pekee ya kufikia lengo lake ni kujilengisha ili kuingia kwenye mahusiano na mwanamziki husika.

Kuonja

Wanawake wanapenda kulakula na wanapenda wanaume ambao wanajua kupika. Kama huamini chunguza migahawa miwili; mmoja kuwe na mpishi wa kiume na mwingine mpishi wa kike kisha angalia ni mgahawa gani una wateja wa kike zaidi ya mwingine.

Wanawake wanavutiwa kwenda kwenye mgahawa wenye mpishi wa kiume ili kujua tu (*out of curiosity*) chakula chake kikoje. Chakula kizuri kilichopikwa na mwanaume kinagusa hisia za wanawake kupitia milango mitatu ya fahamu;

- kwa harufu nzuri puani,
- uzuri wake machoni na
- radha yake ulimini.



Anawaza namna atakavyokuwa anaandaliwa maanjumati kama haya.

Kugusa

Wasanii wengi hususani wa mziki na filamu wana muonekano mzuri wa kimazoezi ambao huwavutia sana wanawake. Ushawahi kuona mwanamke anavyomuangalia au anavyotembeza tembeza mikono au vidole vyake kwenye mwili wa mwanaume wa mazoezi? Nenda kwenye zile sehemu za kufanyia mazoezi maarufu kama gym ujionee maajabu.

Kunusa

Hapa inaingia harufu ya chakula (chakula tushagusia kwenye kipengele cha kuonja) au manukato katika mwili wa mwanaume.



Wanamuziki wenye asili ya Kikongo huwavutia wanawake kwenye mavazi na manukato. Ukitaka kuthibitisha kauli yangu waulize wanawake hapa Dar es salaam.

Yawezekana hauwezi kuimba au kuigiza ila inawezekana;

1. Kujitahidi kufanya mazoezi kuweka mwili kwenye muonekano mzuri.
2. Kujifunza kupika. Inalipa aisee japokuwa wanaume wengi wanaiona ni kama ishu za kike.
3. Kuvaa vizuri. Haina maana iwe nguo za gharama. Usafi tu wa nguo na namna ya kuzipangilia kwenye uvaaji inatosha kumvutia mwanamke wa kiwango chako.
4. Kunukia vizuri. Si lazima manukato ya ghali. Yapo mafuta na manukato ya bei za kawaida ambayo unaweza kuyamudu.
5. Kujifunza kumuambia mkeo maneno mazuri. Na kipimo chepesi cha kujua neno hili ni zuri au baya ni wewe kujiuliza kabla ya kulisema **je neno hili nikiambiwa mimi nitalifurahia au nitachukia**. Ikiwa utalichukia liache, ikiwa utafurahi basi mwambie. Na lau kama utateleza kwa ubinadamu wako na kutamka neno baya, muombe mkeo msamaha kwa kuteleza. Kuomba msamaha ni katika maneno mazuri kwani huonyesha utu wako, kujali na si katika kujishusha kama wanavyodhani wanaume wengi.

SURA YA TANO
ADIVENCHARA
(*Adventurer*)

Adivenchara wanapenda ‘totoz kali’,



Wanapenda ‘ndinga kali’,



Wanapenda kwenda sehemu ‘baab kubwa’ na zenye gharama,



Hizi ni baadhi ya sifa za adivenchara.

Kwao adivenchara, maana ya Maisha ni kuburudika (*having fun*). Na burudani yao ni kufanya mambo ambayo ni ya hatari au hayaingii akili (*crazy stuffs*) ambayo mtu wa kawaida hawezi kuyafanya. Mfano kuendesha magari kwa kasi. Mcheiki Dom kwenye filamu ya *fast furious*.



Adivenchara ni watu wa sapraizi na hakuna viumbe ambao wanapenda sapraizi kama wanawake. Ukitaka kuamini, mfunge mwanamke kitambaa machoni mwake kisha muambie una sapraizi kwa ajili yake. Tegemea kupata tabasamu pana kama la huyu dada;



Tumeona ya kuwa wanawake hupata hisia kupitia milango yote ya hisia. Unapomfunga kitambaa machoni, kiuhalisia unaibua milango yake mingine ya hisia kuanza kufanya kazi. Adivenchara ni mfano wa kitambaa machoni kwa mwanamke. Kwa kuwa Maisha yao ni saprazi (hawatabiliki kwa sababu muda wowote wanaweza kufanya lolote), huwafanya wanawake kuwa na tashiwishi. Kama jana alimfanyia sapraizi ya kumtoa *out* kwa gari moja kali, leo mwanamke anawaza siku itakuwaje. Wanawake hawaboreki kuwa na Adivenchara. Na kwanini waboreke na watu ambao kuwapeleka Dubai kwao sio ishu;



Au kwanini waboreke na wanaume wanaowaendesha kwenye magari kama haya;



Adivenchara ni aina ya mwanaume ambaye hawi na mwanamke mmoja.



Na wanawake wanalijua hilo na ushahidi ni hili swali ambalo kutokana na raha wanazopata kwa wanaume hawa na wivu waliokuwa nao juu yao, huwa wanapenda kuliuliza; “wanawake zako wangapi ushawahi kuwaleta hapa?”.

Adivenchara pia wana tabia ya usaliti na hajali kufumaniwa bali hicho kitendo tu cha kufumaniwa kwake ni burudani hasa pale wanawake wanapoanza kupigana kwa ajili yake mbele

yake. Na si ajabu baada ya ugomvi huo akawaambia, “mmemaliza? Sikilizeni nyinyi wote ni wapenzi wangu na nawapenda ila kama kuna mmoja wenu hawezi kuvumilia mimi kuwa na mwenzake, aondoke” na wanawake wote wakatulia tuli asiondoke hata mmoja wao.



Noma sana hawa jamaa unaweza ukahisi ni wachawi.

Mfano wa filamu zinazoonyesha wanaume wa aina hii ni James Bond. Angalia filamu za Bond, angalia namna tabia zake zilivyo kwa wanawake na angalia namna wanawake wanavyovutiwa nae.



Adivenchara ana hitimisha aina nne za wanaume wenye sifa za Mpenzi.

Na nilisema kwenye sura ya kwanza ya kuwa wanawake wanasukumwa kujamiana haraka sana na aina hizi za wanaume. Kitu pekee ambacho sikukisema ni sababu ya wao kufanya hivyo. Nimeona sababu hii ni hitimishie hapa.

Sababu ni kuwa wanawake ni viumbe vya hisia kama tulivyoona huko nyuma na ukirudia kusoma tena aina hizi nne nilizozitaja utagundua ya kuwa wote wanamgusa mwanamke katika hisia zake, na ndipo udhaifu wake ulipo.

Kuna msembo wa kiingereza usemao *“a way to a man’s heart is through his stomach”* (Tafsiri: Njia ya kuuteka moyo wa mwanaume ni kupitia tumbo lake-wakiimaanisha chakula kizuri)

Nami nasema *“a way to a woman’s heart is through her emotions”* (njia ya kuuteka moyo wa mwanamke ni kupitia hisia zake).

Na wanaume wenye sifa ya MPENZI wanalijua hili.

Sehemu ya pili na sura zinazofata zinaelezea aina nyingine ya wanaume wanaowavutia wanawake wenye sifa ya BUZI ambao ni kinyume cha wanaume wenye sifa za MPENZI.

SEHEMU YA PILI

Buzi

1. Sponsa (*Sponsor*)
2. Dadi (*Daddy*)
3. Bwege/Zoba (*Regular man*)
4. Toi (*Toy boy*)

SURA YA SITA

SPONSA (*Sponsor*)



Anasema mwanamke mmoja, “ninatembea na wanaume matajiri wenye uchu na sijutii kwa hilo”

Sponsa anawakilisha wanaume ambao wamefanikiwa kimaisha anaweza kuwa ni mfanyabiashara au mfanyakazi kama daktari, mwanasheria nakadhalika. Huyu ni aina ya mwanaume ambaye pesa kwake sio tatizo. Wanawake wengi wanajaribu kutafuta wanaume wa aina hii ili waolewe nao au kuwa nao kimahusiano.

Viashiria vya mwanaume sponsa kwa mwanamke ni una usafiri mzuri, unaishi kwenye nyumba nzuri, unamtoa *out* kwa matembezi, chakula au nguo na zawadi zingine.



Sponsa ni katika wanaume ambao wanawakilisha mwanaume mwenye mamlaka (*dominant*).

Kwenye [kidokezo](#) tumeona moja ya majibu wanayotoa wanawake kuhusu aina ya wanaume wanaopenda au kuvutiwa kuwa nao ni wale wenye pesa.

Pesa kwa wanawake inawakilisha;

1. Dhamana ya Maisha yake kutoteteleka (*security*)
2. Usalama wa mahitaji yake kutimizwa (*stability*)

Mwanamke yuko radhi kuwa na mwanaume ambaye ana uhakika wa kupata laki mbili mbili kila mwezi lakini hayuko radhi kuwa na mwanaume mwenye ‘mchongo anausikilizia’ bila kujua ni lini mchongo huo utafanikiwa. Ndio maana mwanaume anaweza kuishi na mwanamke ambaye hana pesa kwa miaka mingi lakini mwanamke hawezi kuishi na mwanaume ambaye hana pesa kwasababu anaona Maisha na mahitaji yake yatateteleka.

Nilisema ya kuwa kuvutiwa kuko kwa namna mbili;

1. Kuvutiwa na mtu alivyo
2. Kuvutiwa na kitu alichonacho mtu

Namna ya kwanza, mara nyingi inaambatana na wanawake kupenda kwa dhati. Na katika hili zinaingia aina zile nne za wanaume wenye sifa ya [MPENZI](#). Namna ya pili inaambatana na wanawake kufeki mapenzi. Mara nyingi, wanaingia katika hili aina nne za wanaume wenye sifa ya [BUZI](#) kama tutakavyoona tukianza na Sponsa.

Sponsa huwavutia wanawake kwa kile walichonacho, nacho ni pesa. Kama ilivyo tabia ya wanaume wengi kutanguliza pesa ili kuwanasa wanawake, masponsa wengi hudhani pesa zao zinatoshwa kuwafanya wanawake wawapende. Ukweli ni kuwa pesa inatoshwa kumnasa mwanamke ila haitoshi kumfanya akupende. Mwanamke anaweza kuishi na mwanaume mwenye pesa kwa miaka mingi bila kuwa na mapenzi nae maadamu ana mchepuko wake ambao anaupenda. Na si ajabu kukuta mchepuko huo huwa kwenye kundi mojawapo la MPENZI tuliyokwisha kuyaona.

Na kwa kuwa kigezo cha mwanamke kuvutiwa na sponsa ni pesa na si mapenzi, kinachotokea ni mwanamke kujizuia kumpa ‘tendo’ sponsa. Na ikitokea amempa, ni kwa sababu ya huduma ya mahitaji anayopata ili kumshajiisha sponsa kuendelea kutoa huduma hiyo. Wakati pekee ambao mwanamke anaweza kutoa tendo kwa sponsa kwa dhati ni pale tu sponsa akiwa na sifa moja au zaidi kati ya zile sifa za wanaume wenye sifa ya MPENZI.

Niligusia katika sura ya kwanza ya kuwa, kutanguliza pesa mbele ili kumnasa mwanamke kutafaa tu ikiwa mwanaume;

1. anatafuta mwanamke wa ‘huduma ya haraka’ kama machangudoa/wadangaji
2. anatafuta mwanamke wa kupitisha siku (*one-night standing*).
3. anatafuta mwanamke wa kustarehe nae tu na kuhonga kwake sio tatizo.

Lakini ikiwa wewe ni Sponsa na unatafuta mwenza wa kimaisha, jaribu kufanyia kazi sifa za adivenchara au mtongozaji au msanii kisha fatisha zile hatua sahihi nilizozitaja. Nitazirudia tena hapa;

1. Jijue wewe ni nani
2. Jua unataka mwanamke wa aina gani
3. Jua mwanamke wa aina unayotaka anapatikana wapi
4. Ongea lugha yake

Nini Cha Kujifunza Kwa Sponsa

1. Heshima ya mwanaume katika familia iko katika kutoa mahitaji. Toa mahitaji kwa mkeo.
2. Kupambana: Kwa mwanaume pesa ni chanzo cha mamlaka (*power*) na utawala (*control*). Mwanaume anapokosa pesa, kwenye fikra zake anapoteza vitu hivi viwili na kumfanya kuwa mnyonge. Pambana.

Nini cha Kuacha kwa Sponsa

1. Usitangulize pesa mbele kama unatafuta mwenza sahihi wa Maisha

SURA YA SABA

DADI

(Daddy)



Mwanamke anasema, “nikiwa nae najihisi kama kabinti kadogo”

Dadi ni aina ya wanaume ambao hupenda kuwafanya wanawake wajihisi kama vibinti vidogo. Mwanaume aina ya dadi anaweza kuwa wa umri wowote kwa sababu kinachozingatiwa katika hili jina ni ile tabia ya kumfanya mwanamke ajihisi kabinti. Hata hivyo wengi katika wanaume wanaoingia kwenye kundi hili ni wale ambao wana umri mkubwa kuliko wanawake wao.

Wakati pesa inaweza kuwa chanzo cha wanawake wenye umri mdogo kuwa kimahusiano na dadi wa umri mkubwa kuliko wao, wanawake wenye pesa hupenda kuwa na dadi ili apate ile hisia ya kudekezwa na kufanywa kama mtoto mdogo.

Dadi anawakilisha;

1. ulinzi (*protection*) kwa mwanamke kama ambavyo kabinti kanavyojihisi kako salama akiwa na baba yake.
2. mwanaume mwenye mamlaka (*dominant*) na utawala (*control*).

Sifa hizi mbili ni katika sifa zinazowavutia sana wanawake.

Na katika zile aina mbili za kuvutia ambazo;

1. Kuvutiwa na mtu alivyo
2. Kuvutiwa na kitu alichonacho mtu

Dadi anaingia kwenye aina ya kwanza. Wakati pekee ambao anaweza kuingia kwenye aina ya pili ni pale ambapo hayuko vizuri faragha.

Kutokana na umri,

1. Dadi wengi hawako vizuri faragha,
2. hawapendi kuwa kimahusiano na wanawake wa rika lao na
3. huvutiwa na wanawake ‘damu changa’.

Ndio maana waswahili wakasema “gari bovu huvutwa ni gari zima”. Na kwa kuwa dadi wengi ni wanaume wenye pesa, wanatumia pesa zao kuwanasa wanawake damu changa kwa sababu wanajua ndizo zinazowavutia. Kwa hiyo kila mmoja anafaidika;

- dadi anakula uzee kwa kuwa na damu changa na
- damu changa anapata pesa za kutanua kimaisha.



Lakini kama ilivyo kwa sponza, mara nyingi hawa wanawake huwa wanachepuka.

Nini Cha Kujifunza Kwa Dadi

1. Kama unaweza kumfanya mkeo ajihisi kama mtoto mdogo, fanya hivyo. Wanawake wanapenda hilo.



2. Dadi ni maarufu kwa kuhonga, kama una uwezo wa kufanya hilo fanya, kwani unataka kumhonga nani kama sio mkeo. Na simaanishi vitu vya gharama bali kwa kadri ya uwezo wako.



Nini cha Kuacha kwa Dadi

1. Kutokana na tabia ya kupenda damu changa, dadi wanaangukia kuwa ‘mafataki’ (*pedophile*) kwa kupenda wasichana wadogo wenye umri wa kwenda shule. Epuka hii tabia, jela itakuhusu.



SURA YA NANE

BWEGE/ZOBA

(Regular guy)



Wanaume wengi wanaingia kwenye aina hii kwa sababu ndiyo inayopatikana na kuzoeleka kwenye jamii sana. Ni aina ambayo mzazi hana tabu kumuoza binti yake.

Ni wanaume ambao wanaamka asubuhi kwenda kujitafutia riziki na kurudi majumbani mwao nyakati za jioni, siku za wikiendi wanakuwa na familia zao, waminifu (wanaweza kuwa na tabia ya usaliti lakini wanajitahidi sana kujificha ili wasijulikane kwa wake zao au jamii), wanaweza kuwa ni watumiaji wa pombe lakini si kiasi cha kupindukia kama *Bad Boy*, sio matajiri lakini wanajitahidi kuhudumia familia zao kwa kadri ya uwezo wao na ni wapenzi wa burudani kama mpira, filamu au kutoka na marafiki kwenda kwenye kumbi za starehe. Bila shaka unawajua wanaume wa aina hii. Jirani yako anaweza kuwa miongoni mwao.

Mwanzo wa mahusiano au kipindi cha ujana wao, mara nyingi wanaume wa aina hii wanaonyesha kuwa na sifa na tabia za adivenchara au mtongozaji kisha kadri mahusiano yanavyosonga mbele au umri unavyoongezeka, wanaanza kuziona tabia au sifa hizo kuwa sizokubalika au kuendana na umri wao au ni maalumu kwa vijana tu na hatimaye hubadilika na kuwa wanaume wa kawaida.

Kama alikuwa anakimbizana na kutekenyana na mkewe mwanzoni mwa ujanani wao au mahusiano yao, anaacha. Kama alikuwa anatoka na mkewe matembezi, anaacha. Kama alikuwa

anatoa maneno mazuri kwa mkewe, anaacha. Bila kujua anajikuta anaacha kila sifa au tabia ambayo ilimfanya mkewe kuvutiwa nae. Hatimaye mwanamke anaanza kuboreka.

Mwanamke akiaanza kuboreka anaweza kufanya moja kati ya haya;

1. Kufanya vituko ili aachike au
2. Ikiwa hataachika au atataka kuendelea kubaki na mwanaume wa aina hii kutokana na maslahi anayopata ya kihuduma/pesa au anataka kuondoa upweke wa kuboreka, ataanza kujitutumua na kuwa sauti ndani ya familia.

Mwanaume wa aina hii anapoanza kuziona tabia ya mwanamke kujitutumua, huwa anamuacha mwanamke afanye anachotaka na hapa ndio uzoba au ubwege unapoaanzia. Mara nyingi hali hii inatokea ikiwa mwanaume 'amekolea' kwenye mapenzi. Na hapa ndipo mwanamke anaanza kuwa mtawala na kuinjoi.



Hali inapofikia hatua hii, tabia kama za kulala nje ya nyumba, kuleta wanaume ndani, kumkalipia, na kumfanyisha kazi za ndani mwanaume, zinaanza kuwa za kawaida kwa mwanamke. Kwa hiyo wanaume sampuli hii wanawavutia wanawake kutokana na ule uhuru wanaoupata kutoka kwao wa kufanya wanachotaka. Kama hutaki kuwa mwanaume Bwege, hakikisha haupotezi kile ambacho kilifanya mkeo akupende na kukubali kuolewa na wewe.

Ni kweli umri unapokwenda kuna baadhi ya mambo hayawezi kufanyika lakini si mengi kiasi cha kuzidi ambayo yanaweza kufanyika, tena ya kawaida na hayazingatii umri kama;

- Kumwambia mkeo maneno mazuri
- Kumtoa matembezi si lazima iwe sehemu ya gharama. Wanawake huwa ni waelewa na si kwamba hawajui umri umekwenda na kuna mambo hayawezi kufanyika kama zamani lakini wanafurahi na kuridhika maadamu unajitahidi kiasi cha uwezo wako.
- Kumlisha mkeo, Nimepata kuona video moja ikionyesha vikongwe wawili (mume na mke) katika mazingira duni kabisa lakini mume anamlisha mkewe. Mke alikuwa anacheka kiasi cha kuonekana mapengo yake,
- Chezacheza na mkeo. Kama mlizoea kutekenyana na unaona aibu kufanya hivyo mbele ya watoto na wajukuu zako, fanya hivyo mkiwa chumbani. Bali kuna michezo mingine ambayo haina athari kwa watoto na inawezekana kufanyika mbele yao, endeleeni kuifanya. Kufanya hivi si tu kunarudisha mapenzi baina yenu bali kunajenga msingi mzuri na mfano bora kwa watoto wa namna ya kuishi na familia zao wakiwa wakubwa.

SURA YA TISA

TOYI

(Toy Boy)



Chukua mdoli (*toy*) uulaze, utalala. Uukalishe, utakaa. Uufanye chochote unachotaka, mdoli unakuitikia.

Wapo wanaume wenye tabia hii. Sio mazoba wala mabwege ila tabia hii inatokana na

- kuwa watiifu sana (*too loyal*) kwa wapenzi zao aidha kwa sababu wanawapenda sana kupitiliza au wanaogopa kuwakwaza au kuwakera kama watasema au kufanya kitu au
- ni wanaume wenye umri mdogo (maarufu kama vibenten) kuliko wanawake zao au
- ni wanaume wanaopenda kulelewa au hawapendi majukumu maarufu kama marioo.

Kwa hiyo wanaona ni bora kunyamaza, kutii na kufanya kile wanachoambiwa ili tu kumridhisha mwanamke wake.

Toy ni aina ya mwanaume ambaye humpa au hufanya kila ambacho mwanamke anakitaka. Toyi anawakilisha wanaume watawaliwa (*submissive*). Sababu zinazoweza kumfanya mwanamke kubaki na mwanaume aina hii ni;

1. Pesa zake ili amchune, kama hana pesa sababu ya pili inahusika



2. Uzuri wa sura yake. Wanawake wanapenda kuwatumia kwa kujionesha (*showing off*) kwa shoga zake akitoka matembezi. Uhusiano wa aina hii mara nyingi haudumu kwani mwanamke humuacha mwanaume toyi mwenye sura nzuri pindi anapopata toyi mwengine kushinda wa kwanza.



3. Uhuru: Kama ilivyo kwa mwanaume aina ya Bwege/Zoba, mwanaume toyi anampa mwanamke uhuru wa kufanya anachokitaka.



Moja ya vituko nilivyopata kuviona kuhusu wanaume wa aina hii ni video moja ya mwanamke ikionesha akijisadia haja kubwa kwenye kinywa cha mwanaume mmoja.

Hebu fikiria utoyi huu.

Sishauri kuwa mwanaume awe wa sampuli hii.

MUHTASARI

1. Kupata mwenza wa Maisha, tumia njia sahihi kwa kufata hatua hizi;

- Jijue wewe ni nani
- Jua unataka mwanamke wa aina gani
- Jua mwanamke wa aina unayotaka anapatikana wapi
- Ongea lugha yake

Hatua hizi zitapelekea mwanamke kukuweka katika kundi la wanaume makini na wenye sifa ya kuwa MPENZI.

2. Usitangulize pesa mbele kumnasa mwanamke. Kutanguliza pesa kunatafsiriwa na wanawake kama hadaa na kunawafanya kukuweka kwenye aina ya wanaume wenye sifa ya kuwa BUZI.

3. Njia ya kutanguliza pesa mbele ili kumnasa mwanamke inafanya kazi;

- Kama unatafuta mwanamke wa 'huduma ya haraka' kama machangudoa/wadangaji
- Kama unatafuta mwanamke wa kupitisha siku (*one-night standing*).
- Kama unatafuta mwanamke wa kustarehe nae tu na kuhonga kwako sio ishu.

4. Kila aina ya wanaume ina faida na changamoto zake, ila mwanaume bora ni mwenye mchanganyiko wa baadhi ya sifa za aina hizi kuendana na wakati;

- kuna wakati wa kumdekeza mwanamke na kumfanya kama mtoto (Dadi),
- kuna wakati unatakiwa kutumia maneno matamu (Msanii),
- kuna wakati unatakiwa kuwa mkali, kufanya maamuzi magumu na mwanaume mwenye mamlaka bila kutumia mabavu ya kupiga na kutesa (Chakaramu/Bad Boy),
- kuna wakati wa kutoka matembezi (Adivenchara),
- kujifunza na kujua tabia za wanawake na hisia zao (Mtongozaji)
- kuhudumia familia yako (Sponsa),
- kuwa mwaminifu (Zoba).

5. Epuka kuwa na sifa ya ubwege au uzoba kiasi cha kumfanya mwanamke afanye anachotaka. Bali epuka kila sifa na tabia mbaya zilizopo kwenye aina hizo.

6. Sishauri kabisa mwanaume kubeba sifa za mwanaume toyi.

KIDOKEZO CHA KITABU KIJACHO

“A way to a woman’s heart is through her emotions” (njia ya kuuteka moyo wa mwanamke ni kupitia hisia zake).

Ni maneno yangu yaliyokuwepo kwenye kitabu changu cha kwanza cha **Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake**.

Katika kitabu kile nilisema wanawake ni viumbe vyenye hisia zaidi kuliko wanawake na sababu pekee inayowafanya wanaume aina zile 8 kuwavutia zaidi wanawake kuliko wanaume wengine ni kwasababu **wanagusa hisia zao ambapo ndipo udhaifu wao ulipo**. Kama hujakisoma kitabu cha *Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake* ni vizuri ukaanza nacho kwani msingi wa kitabu hiki cha pili unachokisoma sasa ulianza kule.



Kitabu hiki **Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake** ni upande mwengine wa shilingi wa wanaume ambao **wanazivuruga na hawajui kuzigusa hisia** za wanawake. Nimekiandika mahususi kwa ajili ya;

1. Kumuonyesha mwanaume kama hakujiona kwenye kitabu cha kwanza cha *Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake* bila shaka anaweza kuwa kwenye aina hizi kwenye kitabu hiki cha pili.
2. Wanaume ambao huambulia ‘vibuti’ kila wanapotongoza wanawake hivyo hujihisi kuwa hawana bahati.
3. Wanaume ambao hawadumu kwenye mahusiano au ndoa zao. Kila akiwa na mwanamke baada ya muda tu mahusiano au ndoa huvunjika

Ninatumai kupitia kitabu hiki wanaume wote watakojikuta wapo kwenye mojawapo ya aina hizi watachukua hatua za;

1. kubadilisha tabia zao ili kudumisha ndoa na mahusiano yao na wake zao.
2. Kubadilisha tabia zao na kuwa wanaume wenye bahati ya kupata wake wa ndoto zao na kusahau ‘vibuti’

Ungana nami.

PATA NAKALA YAKO

KUHUSU MWANDISHI

Shamte Kilalile anaishi Dar es Salaam, Tanzania na ni mhitimu wa shahada ya Uchumi na Mipango kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, Morogoro. Amebobeza katika Ujasiriamali, Masoko, Uandishi wa Matangazo (*Copywriting*), Uandishi wa vitabu na Uandishi wa miswada ya filamu. Na ni mwanagenzi katika fani ya *Coding*.

Ni mwanzilishi wa SparkCopy na anatoa huduma za;

1. uandishi wa riwaya (*novels*), vitabu vya biashara/ujasiriamali au miswada ya filamu (*scripts*) kwa watu wenye stori au mawazo vichwani mwao lakini hawezi kuandika vitabu au miswada kwa ajili ya filamu wanazotaka kuzitengeneza.
2. uandishi wa matangazo ya redio, televisheni, kubrandi ukurasa wa LinkedIn, *motivation letter* au *statement of purpose* kwa wanafunzi wanaokwenda vyuo vikuu vya nje na *cv/resume*.

Kujua zaidi huduma hizi tembelea tovuti <https://sparkcopy.wordpress.com/>

Ni mtaalamu wa masoko (*marketing consultant*) na anatoa huduma kwa wafanyabiashara wanaohitaji msaada kubusti masoko kwa ajili ya biashara zao. Kujua zaidi huduma hii tembelea tovuti: <https://yourmarcon.wordpress.com/>

Ni dalali wa kujitegemea (*independent realtor*) wa nyumba, viwanja, mashamba, hoteli, shule na vituo vya mafuta jijini Dar es Salaam kwa njia ya mtandao. Kama atakuwa hajihusishi na uandishi wa vitabu, utaalamu wa masoko basi atakuwa akijishughulisha na shughuli hii. Kupata huduma hii tembelea tovuti: <https://estateowners.wordpress.com/>

Pia ni mwandishi wa muswada wa show ya burudani, elimu na michezo cha iitwayo luninga **GAME ON**. Demo ya show iko [Youtube](#).

Kwa mrejesho umekionaje kitabu hiki, swali kuhusu huduma nilizotaja au ukitaka kuoda kitabu kingine

Piga simu: +255718515321/+255759694551

Barua pepe: rkilalile@gmail.com

KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE

Vitabu vya Riwaya

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Msaliti](#)
3. [Mpango Kabambe](#)

Vitabu vya Simulizi Fupi

1. Natamani Kukusahau
2. Isn't Such A Bad Idea

Vitabu vya Mahusiano & Mapenzi

1. Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake (Kitabu cha Pili)

Miswada ya Filamu

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Mpango Kabambe](#)
3. [100](#) (lugha ya Kiingereza)

Vitabu vya Biashara

1. [Personal Guide: How to Become an Entrepreneur](#)